JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE (SFNA) 2024

## KISWAHILI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE (SFNA) 2024

## 01 KISWAHILI

*Kimechapishwa na;*

Baraza la Mitihani la Tanzania,

S.L.P. 2624,

Dar es Salaam, Tanzania.

© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2024

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO

DIBAJI ........................................................................................ iv

1.0 UTANGULIZI ........................................................................ 1

2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI ............................ 2

2.1 Sehemu A: Imla .................................................................. 3
2.2 Sehemu B: Uundaji wa maneno ............................................ 9
2.3 Sehemu C: Nahau ................................................................ 14
2.4 Sehemu D: Uandishi wa barua ............................................ 19
2.5 Sehemu E: Ufahamu ............................................................ 26

3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WANAFUNZI KATIKA KILA UMAHIRI ........................................................................ 33

4.0 HITIMISHO ........................................................................ 34

5.0 MAPENDEKEZO ................................................................ 34

KIAMBATISHO NA.1: UFAULU WA WANAFUNZI KWA KILA UMAHIRI

KATIKA SFNA 2024 ................................................................ 37

KIAMBATISHO NA.2: ULINGANIFU WA UFAULU WA WANAFUNZI KWA KILA UMAHIRI KATIKA SFNA 2024 NA SFNA 2023 ................. 38

# DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania limeandaa taarifa ya uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne kwa somo la Kiswahili mwaka 2024. Lengo la taarifa hii ni kutoa mrejesho kwa walimu, wanafunzi, watunga sera, wathibiti ubora wa shule, watunga mitaala na wadau wengine wa elimu kuhusu sababu zilizochangia ufaulu wa wanafunzi katika somo la Kiswahili. Vilevile, uchambuzi huu unaonesha jinsi ufundishaji na ujifunzaji ulivyomwezesha mwanafunzi kupata maarifa stahiki kwa kipindi cha miaka minne.

Ripoti hii imechambua mambo mbalimbali yaliyochangia baadhi ya wanafunzi kushindwa kujibu maswali kwa usahihi. Baadhi ya mambo hayo ni kushindwa kuelewa matakwa ya swali, kukosa maarifa ya kutosha kuhusu swali husika na athari ya lugha mama. Majibu ya wanafunzi kwa kila swali yameainishwa katika uchambuzi kwa kutumia vielelezo, chati na maelezo.

Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa taarifa hii itawawezesha walimu wa somo la Kiswahili na wasimamizi wa elimu kubuni mbinu zitakazosaidia kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili kwa lengo la kutatua changamoto zilizobainishwa katika ripoti hii. Vilevile, Baraza la Mitihani la Tanzania linategemea kuwa maoni yaliyotolewa yakifanyiwa kazi, yatasaidia kuongeza umahiri wa wanafunzi na hatimaye kuimarisha ubora wa elimu nchini.

Baraza la Mitihani la Tanzania linatoa shukurani za dhati kwa wote walioshiriki kuandaa taarifa hii.

Prof. Said A. Mohamed
**KATIBU MTENDAJI**

# 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii inatoa mrejesho wa namna ambavyo wanafunzi walijibu maswali katika Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne katika somo la Kiswahili kwa mwaka 2024. Upimaji ulizingatia matakwa ya muhtasari wa mwaka 2015 unaolenga kuimarisha umahiri wa mwanafunzi katika Stadi za Kuzungumza, Kusikiliza, Kusoma na Kuandika.

Upimaji wa somo la Kiswahili ulikuwa na sehemu tano (A, B, C, D na E). Sehemu A ilipima umahiri wa mwanafunzi katika kusikiliza matamshi ya silabi, maneno, sentensi na kuyaandika (imla), Sehemu B ililenga kupima umahiri wa mwanafunzi katika kuunda maneno ya Kiswahili kwa njia ya udondoshaji wa silabi. Sehemu C ililenga kupima umahiri wa mwanafunzi wa kuandika maana za nahau alizopewa. Sehemu D ilipima umahiri wa mwanafunzi katika uandishi wa barua ya kirafiki kwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi kwenye barua husika. Sehemu E ilipima umahiri wa mwanafunzi katika kusoma habari na kisha kujibu maswali ya ufahamu aliyopewa. Sehemu hizo zilitoka katika umahiri mkuu wa *Kuwasiliana katika Miktadha Mbalimbali* na *Kuonesha Uelewa wa Jambo Alilolisikiliza au Kulisoma*. Kila sehemu (A, B, C, D na E) ilikuwa na swali moja (1) lenye vipengele vitano (5) vyenye alama kumi (10).

Jumla ya wanafunzi 1,633,272 walisajiliwa kufanya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne mwaka 2024. Kati yao, wanafunzi 1,530,614 walifanya upimaji katika somo la Kiswahili ambapo wanafunzi 1,293,605 sawa na asilimia 84.51 walifaulu upimaji huo.

Viwango vya ufaulu vya majibu ya wanafunzi vimegawanywa katika makundi mawili kulingana na alama walizopata. Kundi la kwanza linahusisha swali la 1 na 5 ambapo kiwango hafifu cha ufaulu ni kati ya alama 0 - 2.5, wastani ni 3.0 - 6.0, kizuri 6.5 - 9.5 na kizuri sana ni alama 10. Kundi la pili linahusisha swali la 2, 3 na 4, kiwango hafifu ni alama 0 – 2.0, wastani ni alama 4.0 - 6.0, kizuri ni alama 8.0 na kizuri sana ni alama 10. Wanafunzi waliopata kuanzia kiwango cha wastani hadi kiwango kizuri sana ndio waliotajwa kuwa wameweza kujibu maswali kwa usahihi. Aidha, waliopata kiwango hafifu wanatajwa kuwa wameshindwa kujibu maswali kwa usahihi.

Uchambuzi wa takwimu za ufaulu wa wanafunzi katika kila swali umewasilishwa kwa njia ya chati. Rangi mbalimbali zimetumika kubainisha asilimia ya ufaulu wa wanafunzi kwa kila swali. Rangi nyekundu inawakilisha kiwango hafifu cha ufaulu wa asilimia 0 – 33, rangi ya njano kiwango cha wastani wa asilimia 34 – 66 na rangi ya kijani inawakilisha kiwango kizuri na kizuri sana cha asilimia 67 – 100.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI

Sehemu hii inachambua majibu ya wanafunzi kwa kila swali. Aidha, idadi na asilimia ya wanafunzi waliojibu vizuri au walioshindwa kujibu kwa usahihi imeoneshwa katika chati. Vilevile, taarifa imeonesha sababu za ufaulu wa wanafunzi kwa kila swali. Sampuli za majibu ya baadhi ya wanafunzi zimetumika kuonesha viwango vya ufaulu hafifu, wastani na mzuri katika maswali.

## 2.1 Sehemu A: Imla

Sehemu hii ilikuwa na swali moja la imla ambalo lilitoka katika umahiri mkuu wa *Kuwasiliana katika Miktadha Mbalimbali*. Wanafunzi walitakiwa kusikiliza kwa makini sentensi tano (05) walizosomewa kwa sauti kisha walitakiwa waziandike kwa usahihi katika nafasi iliyoachwa wazi. Kila sentensi ilikuwa na maneno manne yenye alama nusu ($00^1/_2$) kwa kila neno. Hivyo, kufanya sehemu hii kuwa na jumla ya alama 10.

Swali lililenga kupima umahiri wa mwanafunzi wa kusikiliza na kuandika sentensi kwa kuzingatia kanuni za uandishi kama vile; kuanza na herufi kubwa mwanzoni mwa sentensi, kuweka alama ya nukta mwishoni mwa sentensi pamoja na kutambua sauti mbalimbali za matamshi ya silabi, maneno na sentensi. Swali hilo lilikuwa kama ifuatavyo:

**Swali la 1**: **Sikiliza kwa makini sentensi zifuatazo kisha uziandike kwa usahihi** katika nafasi zilizoachwa wazi.

(i) ______________________________

(ii) ______________________________

(iii) ______________________________

(iv) ______________________________

(v) ______________________________

Zifuatazo ni sentensi walizosomewa wanafunzi:

(i) Ng'ombe wetu ni mkali.


(ii) Kaka yangu anafua vyuma.

(iii) Dhahabu nzuri hupatikana Mwadui.

(iv) Mtoto huyu alifyeka majani.

(v) Thamani ya dola imepanda.

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 1,530,615 (100%). Kiwango cha ufaulu cha wanafunzi katika swali hili kilikuwa kizuri kwani wanafunzi 1,320,420 (86.27%) walifaulu kwa kupata alama kuazia 3 mpaka 10. Chati Na. 1 inaonesha viwango vya ufaulu vya wanafunzi hao kwa asilimia.





**Chati Na. 1:** *Asilimia ya ufaulu wa wanafunzi katika swali la 1*

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa, wanafunzi 372,175 (24.32%) walijibu swali hili vizuri sana kwani waliweza kuandika maneno yote ishirini kwa usahihi. Hii inaonesha kuwa wanafunzi hao walikuwa na umahiri wa kutosha katika stadi ya kusikiliza na kuandika kwa sababu waliweza kuandika kwa usahihi sentensi zote tano walizosomewa. Pia, walikuwa na umahiri wa kubaini sauti zinazounda maneno yaliyosomwa na kuziandika kwa usahihi huku wakizingatia kanuni za uandishi, kuandika herufi sahihi (fonimu) za maneno husika, matumizi ya herufi kubwa

mwanzoni mwa sentensi na kuweka alama ya kituo mwishoni mwa sentensi.

Vilevile, wanafunzi hao walikuwa na umahiri mzuri wa kubaini na kuandika silabi zenye herufi mwambatano kama “*ng’o’’*, “mbe*’’,* “*ngu’’, “nzu’, “mwa”, “vyu*”, “*dha*”, ‘‘*fye’’,* ‘‘*nda”*` na ‘‘*tha”* kwenye maneno kama “*ng’ombe*”, “yangu“, “Mwadui” “vyuma”, “*dhahabu*”, “nzuri” “fyeka”, “thamani” na “imepanda”. Maneno hayo ni miongoni mwa maneno yaliyounda sentensi tano walizosomewa. Hata hivyo, pamoja na wanafunzi hao kufanya vizuri sana na kupata alama 10, wanafunzi 712,383 (46.54%) walifanya vizuri kwa kupata alama 6.5 hadi 9.5. Wanafunzi hao, waliweza kuandika kwa usahihi maneno 13 hadi 19 kati ya maneno 20. Kielelezo Na. 1.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kuandika kwa usahihi sentensi zote tano na kupata alama zote 10.



1. **Sikiliza kwa makini sentensi zifuatazo kisha uziandike kwa usahihi** katika nafasi zilizoachwa wazi.

(i) Ng’ombe wetu ni mkali.
(ii) Kaka yangu anafua vyuma.
(iii) Dhahabu nzuri hupatikana Mwadui.
(iv) Mtoto huyu alifyeka majani.
(v) Thamani ya dola imepanda.

**Kielelezo Na. 1.1**: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 1

Uchambuzi zaidi wa majibu unaonesha kuwa, jumla ya wanafunzi 235,862 (15.41%) walipata alama za wastani. Wanafunzi hao, walipata alama kuanzia 03 hadi 06, kwani waliweza kuandika kwa usahihi maneno kuanzia 6 hadi 12 kati ya maneno 20. Aidha,

walishindwa kuandika baadhi ya maneno yenye silabi za herufi mwambatano. Kwa mfano, baadhi ya wanafunzi badala ya kuandika neno “Ng’ombe” waliandika “*ngombe*”, “vyuma” waliandika “*viuma”,* “Mwadui” waliandika “madui”. Pia, wanafunzi wengine walishindwa kuandika herufi mwambatano “dh” kwenye neno “dhahabu” waliandika “zahabu”, sauti “th” kwenye neno “thamani” waliandika “samani”, sauti “fy” kwenye neno “fyeka” waliandika “fieka” na “fiyeka”. Wengine walishindwa kuzingatia alama za uandishi kwani walianza kuandika sentensi kwa herufi ndogo mwanzoni mwa sentensi badala ya herufi kubwa pia hawakuweka nukta mwishoni mwa sentensi. Pia katika jina la mji “Mwadui” baadhi hawakuanza kuandika kwa herufi kubwa kama utaratibu wa majina ya pekee inavyopaswa kuandikwa popote yanapotokea katika sentensi. Hivyo, wanafunzi hao walipata alama za wastani katika swali hili. Kielelezo Na. 1.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyepata alama za wastani katika swali la 1.



1. **Sikiliza kwa makini sentensi zifuatazo kisha uziandike kwa usahihi** katika nafasi zilizoachwa wazi.

(i) Ng'ombe wetu nimkali

(ii) kaka yangu anafua Jumo

(iii) Thahaba mzuri hupatikana ma duhi

(iv) Mdolo huyu alifeka magani.


(v) Samani ya dora imepanda.

**Kielelezo Na. 1.2:** Sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyepata alama za wastani katika swali la 1

Kielelezo Na.1.2 kinaonesha mwanafunzi aliyeweza kuandika kwa usahihi maneno 10 kati ya 20. Maneno mengine 10 kati ya 20 hayakufuata taratibu za uandishi wa kuanza na herufi kubwa mwanzoni mwa sentensi kwa mfano neno “Ng’ombe” na “Kaka”. Pia neno la mji “Mwadui” halikuanza kwa herufi kubwa na limekosewa kwa kuandikwa “maduhi”. Maneno mengine yaliyokosewa ni; mkali limeandikwa “mkari”, vyuma limeandikwa “Juma”, dhahabu limeandikwa “Thahaba”, nzuri limeandikwa “mzuri”, alifyeka limeandikwa “alifeka”, thamani limeandikwa “Samani” na dola limeandikwa “dora”. Pia, hakuweka vituo mwishoni mwa sentensi ya (i) hadi (iii). Kutokana na mapungufu hayo mwanafunzi huyu alipata alama za wastani ambazo ni 05 kati ya alama 10.

Aidha, wanafunzi 210,195 (13.73) walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kwa sababu walishindwa kuandika kwa usahihi maneno waliyosomewa. Baadhi yao hawakuacha nafasi kati ya neno moja na lingine, wengine walitenganisha silabi moja na silabi nyingine katika neno. Aidha, wengine waliandika maneno bila kuzingatia kanuni za uandishi ambapo walichanganya herufi kubwa na ndogo ndani ya neno moja. Vilevile, wapo walioanza na herufi ndogo mwanzoni mwa neno. Wengine walishindwa kuandika maneno yenye herufi mwambatano kwa mfano badala ya sauti ***dh*** waliandika “z”, **th** waliandika “s”, silabi ***fye*** waliandika “fe”, “fie” na “fiye”, ***vyu*** waliandika “viu”, “viyu”, “vu” na ***mwa*** waliandika “ma”. Aidha, wengine hawakuweka vituo mwishoni mwa sentensi, na wengine baadhi waliweka alama ya vituo pacha (:) mwishoni mwa sentensi. **Kielelezo Na. 1.3** kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kuandika majibu kwa usahihi. Hivyo

alipata maneno matatu (03) pekee yenye jumla ya alama 1.5 kati ya 20.



1. **Sikiliza kwa makini sentensi zifuatazo kisha uziandike kwa usahihi** katika nafasi zilizoachwa wazi.

(i) ng'mbe we ty ni mkali:

(ii) Kaka yanyuvyuma:

(iii) dha ha Bu ni Mzui uBatikuna kuaDii:

(iv) Mtoto u ya alifuka majo ni:

(v) Sahani yadola inipanda

**Kielelezo Na. 1.3:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 1

Kielelezo Na.1.3 kinaonesha majibu ya mwanafunzi ambaye ameshindwa kuandika herufi mwambatano “ng” kwenye sentensi namba (i), “mw” kwenye sentensi namba (iii) na “th” kwenye sentensi namba (v). Pia amechanganya herufi kubwa na ndogo kwa mfano kwenye maneno “ng’ombe” na ”dola”. Vilevile, hajaacha nafasi kati ya neno moja na lingine kwa mfano neno “yadola” ameunganisha silabi “ya” na neno “dola” Pia ametenganisha silabi za neno moja kwa mfano neno “dhahabu” ameandika “dha ha bu”. Hajaweka kituo (nukta) kwenye sentensi namba (v). Pia ameweka vituo pacha (:) mwishoni mwa sentensi namba (i) – (iv) badala ya nukta (.). Hivyo, mwanafunzi huyu alipata alama 02 kati ya 10 hali iliyodhihirisha kuwa hakuwa na maarifa ya kutosha ya namna ya kutumia alama za uandishi katika sentensi.

## 2.2 Sehemu B: Uundaji wa maneno

Sehemu hii ilikuwa na swali moja lenye vipengele vitano (5). Swali lilitoka katika umahiri mkuu wa *kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza au kulisoma*. Kila kipengele kilikuwa na alama mbili (02), hivyo, swali lilikuwa na jumla ya alama kumi (10). Swali lilipima uwezo wa mwanafunzi katika kuunda maneno mapya kwa kudondosha silabi moja katika kila neno alilopewa kwenye swali. Swali hili lilikuwa kama ifuatavyo:

**Swali la 2**: Andika neno jipya linaloundwa kwa kudondosha silabi moja katika kila neno ulilopewa.

(i) Mkasi____________________________________


(ii) Wazima__________________________________

(iii) Elewa____________________________________

(iv) Mpeni____________________________________


(v) Hatibu____________________________________

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 1,530,615 (100%). Swali lililenga kupima umahiri wa mwanafunzi wa kuunda maneno mapya kwa kudondosha silabi moja kutoka kwenye kila neno alilopewa katika swali la upimaji. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani ambapo wanafunzi 819,407 (53.53%) walipata alama kuanzia 4 hadi 10. Chati Na. 2 inaonesha viwango na asilimia ya ufaulu wa wanafunzi.




**Chati Na. 2:** *Asilimia ya ufaulu wa wanafunzi katika swali la 2*

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa wanafunzi 558,612 (36,50%) waliweza kuunda maneno mapya kwa usahihi kwa kudondosha silabi moja kutoka katika kipengele cha i-v alichopewa hivyo, kupata alama zote kumi (10). Wanafunzi hao walikuwa na umahiri mkubwa wa kuelewa dhana ya udondoshaji wa silabi katika neno na kuunda neno jipya moja au zaidi katika kila kipengele. Hata hivyo, pamoja na wanafunzi hao kufanya vizuri sana na kupata alama 10, wanafunzi 125,112 (8.17%) walikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwani waliweza kuunda maneno sahihi manne kwa njia ya udondoshaji na kupata alama 08. Kielelezo Na. 2.1 ni sampuli ya majibu mazuri katika swali la 2.



2. Andika neno jipya linaloundwa kwa kudondosha silabi moja katika kila neno ulilopewa.

(i) Mkasi Kasi

(ii) Wazima zima/wazi

(iii) Elewa lewa


(iv) Mpeni mpe/peni

(v) Hatibu tibu

**Kielelezo Na. 2.1:** Sampuli ya majibu mazuri katika swali la 2

Kielelezo Na. 2.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kubaini kwa usahihi namna ya kuunda maneno mapya kwa kudondosha silabi moja.

Aidha, wanafunzi 135,683 (8.86%) walipata alama za wastani. Waliweza kuunda maneno kati ya mawili hadi matatu kwa njia ya kudondosha silabi moja kutoka kwenye maneno ya msingi waliyopewa. Wanafunzi hao walikuwa na uelewa wa kiwango cha wastani kuhusu dhana ya silabi kwa sababu baadhi yao walidondosha herufi badala ya silabi. Wengine walidondosha silabi ambayo haikustahili kudondoshwa. Hivyo, kuunda maneno yasiyo leta maana katika lugha ya Kiswahili. Baadhi walidondosha silabi za mwisho kwenye vipengele vyote vitano (5) vya swali bila kujali aina ya neno analoliunda. Kielelezo Na. 2.3 kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyepata alama za wastani kutokana na kudondosha baadhi ya silabi zisizostahili.



2. Andika neno jipya linaloundwa kwa kudondosha silabi moja katika kila neno ulilopewa.

(i) Mkasi Hko

(ii) Wazima Wazi

(iii) Elewa Ele

(iv) Mpeni Mpe

(v) Hatibu Hati


**Kielelezo Na. 2.2:** Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyepata alama za wastani katika swali 2

Kielelezo Na. 2.2 kinaonesha mwanafunzi aliyepata alama za wastani kwa kuunda maneno matatu kati ya matano kwa usahihi katika vipengele cha (ii), (iv) na (v). Aidha, alishindwa kuunda maneno sahihi katika kipengele cha (i) na (iii). Kwa mfano, (i) mkasi; mwanafunzi alidondosha silabi ya mwisho “si” akapata neno “mka” badala ya kudondosha silabi ya kwanza “m (iii) elewa; alidondosha silabi ya mwisho “wa” akapata neno “ele” badala ya kudondosha silabi ya kwanza “e”. Hivyo, katika kipengele (i) na (iii) alipata maneno yasiyo na maana katika lugha ya Kiswahili. Hii inaonesha mwanafunzi huyu hakujengewa uwezo wa kutosha wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa uundaji wa maneno kwa njia ya kudondosha silabi.

Kwa upande mwingine, wanafunzi 711,208 (46.47%) walishindwa kuunda majina mapya kwa kutumia njia ya udondoshaji wa silabi moja. Hivyo, walipata alama za kiwango hafifu kuanzia 00 hadi 02. Baadhi yao waliandika umoja ama wingi wa neno kwa mfano, “mkasi” waliandika “mikasi”, wengine waliandika ukanushi (kinyume) cha neno walilopewa. Kwa mfano, neno “wazima”

waliandika “si wazima” neno “elewa” waliandika “sielewi”, neno “mpeni” waliandika “simpi” na neno “hatibu” waliandika “anatibu”.

Wengine walidondosha irabu zote katika neno na kuacha konsonanti tu. Kwa mfano, katika neno “mkasi” waliandika “mks” neno “wazima” waliandika “wzm” neno “mpeni” waliandika “mpn” na katika neno “hatibu” waliandika “htb”. Wengine walitenganisha konsonanti na irabu katika neno, kwa mfano, “wazima” waliandika “w+a+z+i+m+a”. Aidha, wengine walitunga sentensi kwa kutumia maneno waliyopewa badala ya kudondosha. Wapo waliobadili mpangilio wa herufi na kupata neno tofauti na walilopewa. Kwa mfano, “wazima” waliandika “maziwa”, wengine walibuni maneno yao wenyewe na kuyaandika katika nafasi zilizoachwa wazi kwa mfano, “Waziri” kwenye neno “wazima” na “Eliza” kwenye neno “elewa”. Hii inaonesha kuwa wanafunzi hao hawakuwa na uelewa wa kanuni ya uundaji wa maneno mapya kwa njia ya udondoshaji wa silabi kutoka kwenye neno. Pia, walikosa uelewa wa dhana ya silabi katika neno hali iliyowasababishia wanafunzi hao kupata alama 00 hadi 02 kati ya alama 10. Kielelezo Na. 2.3 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kukidhi matakwa ya swali la 2.


2. Andika neno jipya linaloundwa kwa kudondosha silabi moja katika kila neno ulilopewa.

(i) Mkasi mKas

(ii) Wazima wazim

(iii) Elewa Elow

(iv) Mpeni mpen

(v) Hatibu Hatib

**Kielelezo Na. 2.3**: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 2

Kielelezo Na. 2.3 kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kwa usahihi swali la pili kwani badala ya kudondosha silabi moja, alidondosha irabu ya mwisho kwa kila neno na kuunda maneno yasiyokuwa na maana. Hivyo, alipata alama 00 katika swali hili.

## 2.3 Sehemu C: Nahau

Sehemu hii ilikuwa na swali moja lenye vipengele vitano (5) ambalo lilitoka katika umahiri mkuu wa *Kuwasiliana katika Miktadha Mbalimbali*. Swali lililenga kupima umahiri wa mwanafunzi wa kueleza maana zilizomo kwenye nahau zilizoorodheshwa. Jumla ya alama katika swali hili zilikuwa 10 ambapo kila kipengele kilikuwa na alama 02. Swali liliuliza kama ifuatavyo:

**Swali la 3:** Andika maana ya nahau katika (i)-(v) kwa kuchagua jibu sahihi kutoka kwenye kisanduku na kuliandika katika nafasi iliyoachwa wazi.

| |
|---|
| tamani kitu, ipo siku utakamatwa, kuishi miaka mingi, ona aibu, mwisho wa safari, fukuzwa kazi, kuiba kitu. |

(i) Tia nanga ______________________

(ii) Mezea mate ______________________


(iii) Mwaga unga ______________________

(iv) Kula chumvi nyingi ______________________

(v) Ona haya ______________________

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 1,530,615 (100%). Swali lililenga kupima umahiri wa mwanafunzi katika kutoa maana za nahau


mbalimbali. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri ambapo wanafunzi 1,082,201 (70.70%) waliweza kujibu vizuri. Chati Na. 3 inaonesha viwango vya ufaulu na asilimia ya wanafunzi.




**Chati Na. 3**: *Asilimia ya ufaulu wa wanafunzi katika swali la 3*

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa wanafunzi 298,277 (19.49%) walikuwa na kiwango kizuri sana cha ufaulu. Wanafunzi hao walikuwa na umahiri wa kutosha wa kufahamu maana mbalimbali za nahau hali iliyowasababishia waweze kuhusianisha nahau na mazingira. Hivyo, kuwa rahisi katika kuchagua majibu sahihi kwa kila nahau waliyopewa katika vipengele vyote vitano (5). Kwa mfano, nahau "*Tia nanga*" hapa wanafunzi wamehusisha mazingira ya bandarini pale ambapo meli hufika mwisho wa safari. "*Mezea mate*" hapa wamehusisha kitendo cha mtu kuwa na hamu ya kupata kitu fulani anachokiona kwa wakati ule. "*Mwaga unga*" hapa wamehusisha na kukosa kitu ambacho kilikuwa ni tegemeo lake katika kumpatia riziki. "*kula chumvi nyingi*" hapa wamehusisha na umri mkubwa wa mtu. "*Ona haya*" hapa wamehusisha na kitendo cha mtu kutahayari baada ya

kufanya au kufikiwa na tukio lililomgusa. Hata hivyo, pamoja na wanafunzi hao kufanya vizuri sana na kupata alama 10, wanafunzi 268,363 (17.53%) walipata kiwango kizuri cha ufaulu. Wanafunzi hao, walipata alama 08 kati ya 10 kwani walijibu kwa usahihi vipengele vinne vya swali. Kwa ujumla, wanafunzi hawa walionesha uwezo mkubwa wa kuhusisha nahau na maana zake katika swali husika. Kielelezo Na. 3.1 ni sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika swali la 3.


3. Andika maana ya nahau katika (i) – (v) kwa kuchagua jibu sahihi kutoka kwenye kisanduku na kuliandika katika nafasi iliyoachwa wazi.

| |
|---|
| tamani kitu, ipo siku utakamatwa, kuishi miaka mingi, ona aibu, mwisho wa safari, fukuzwa kazi, kuiba kitu. |

(i) Tia nanga mwisho wa safari.
(ii) Mezea mate tamani kitu.
(iii) Mwaga unga fukuzwa kazi.
(iv) Kula chumvi nyingi kuishi miaka mingi.
(v) Ona haya ona aibu.

**Kielelezo Na. 3.1:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 3

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, wanafunzi 515,561 (33.68%) walipata alama za wastani kuanzia 04 hadi 06 kwa kuwa walikuwa na umahiri mdogo wa kuhusianisha nahau na mazingira mbalimbali. Hivyo, waliweza kuandika kwa usahihi nahau mbili hadi tatu. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja aliweza kuandika kwa usahihi kipengele cha (ii) *mezea mate* kuwa ni “tamani kitu”, (iii) *mwaga unga* kuwa ni “fukuzwa kazi” na kipengele cha (iv) *kula chumvi nyingi* kuwa ni “kuishi miaka mingi”. Hata hivyo, alishindwa kukamilisha kwa usahihi kipengele cha (i) *tia nanga kwakuwa* aliandika kuwa ni

"*fukuzwa kazi*" badala ya "mwisho wa safari" na kipengele cha (v) *ona haya* aliandika kuwa ni "tamani kitu" badala ya "ona aibu". Kielelezo Na. 3.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyepata alama za wastani.

3. Andika maana ya nahau katika (i) – (v) kwa kuchagua jibu sahihi kutoka kwenye kisanduku na kuliandika katika nafasi iliyoachwa wazi.

| |
|---|
| tamani kitu, ipo siku utakamatwa, kuishi miaka mingi, ona aibu, mwisho wa safari, fukuzwa kazi, kuiba kitu. |


(i) Tia nanga fukuzwa kazi
(ii) Mezea mate Tamani kitu
(iii) Mwaga unga Ipo siku utakamatwa
(iv) Kula chumvi nyingi kuishi miaka mingi
(v) Ona haya Ona aibu

**Kielelezo Na. 3.2:** Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyepata alama za wastani

Kielelezo Na. 3.2 kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyepata alama za wastani kwa kuweza kuandika kwa usahihi maana ya nahau katika kipengele cha (ii), (iv) na (v) na kushindwa kipengele cha (i), na (iii) hivyo kupata alama 06 kati ya alama 10 za swali.

Kwa upande mwingine, wanafunzi 448,414 (29.30%) walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 00 hadi 02. Baadhi yao walibuni majibu na kuyaandika kwenye nafasi zilizoachwa wazi. Wengine waliandika wingi wa nahau walizopewa. Pia, wapo waliorudia kuziandika nahau hizo. Vilevile, wapo walioweza kuandika kwa usahihi maana ya nahau moja kati ya tano walizopewa. Wengine waliandika majibu kinyume na matakwa ya swali kama vile; "*tia nanga*" "*ipo siku utakamatwa*" na "*fukuzwa*

*kazi*”, badala ya “mwisho wa safari”.“*Mezea mate*” baadhi walijibu “*kuiba kitu*” na “*ona aibu*”, badala ya “tamani kitu”. Nahau “*mwaga unga*” walijibu kuwa ni “*kuishi miaka mingi*” na“*mwisho wa safari*”, badala ya “fukuzwa kazi”. “*Kula chumvi nyingi*” waliandika “*mwisho wa safari*” na *ipo siku utakamatwa*”, badala ya “kuishi miaka mingi”. Vilevile, katika nahau “*ona haya*” wapo waliojibu “*kuiba kitu*” na “*tamani kitu*” badala ya “ona aibu”. Majibu haya kama yalivyochaguliwa na wanafunzi yanaonesha dhahiri kuwa wanafunzi hawakujengewa uwezo wa kutosha wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa dhana ya nahau na maana zake. Hivyo, kushindwa kujibu kwa usahihi swali husika. Kielelezo Na. 3.3 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu kinyume na matakwa ya swali.


3. Andika maana ya nahau katika (i) – (v) kwa kuchagua jibu sahihi kutoka kwenye kisanduku na kuliandika katika nafasi iliyoachwa wazi.

tamani kitu, ipo siku utakamatwa, kuishi miaka mingi, ona aibu, mwisho wa safari, fukuzwa kazi, kuiba kitu.

(i) Tia nanga kuibakitu
(ii) Mezea mate ona aibu
(iii) Mwaga unga mwisho wa safari
(iv) Kula chumvi nyingi kuishi miaka mingi
(v) Ona haya kufukuzwa kazi

**Kielelezo Na. 3.3**: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 3

Kielelezo Na. 3.3 kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele cha (i), (ii), (iii) na (v) na kupata kipengele cha (iv). Hivyo, kupata alama 02 kati ya alama 10.

2.4 **Sehemu D: Uandishi wa barua**

Sehemu hii ilikuwa na swali moja lenye vipengele vitano (5) ambapo kila kipengele kilikuwa na alama 02 na kufanya jumla ya alama 10. Swali lilitoka katika umahiri wa *kuwasiliana katika miktadha mbalimbali* na lililenga kupima umahiri wa mwanafunzi wa kuandika barua ya kirafiki. Swali lilikua kama ifuatavyo:

**Swali la 4:** Kamilisha barua ya kirafiki ifuatayo kwa kuchagua jibu sahihi kutoka kwenye kisanduku kisha kuandika katika nafasi zilizoachwa wazi.

| |
|---|
| Mimi mdogo wako, Madhumuni ya barua, Shule ya Msingi Ushindi, Ni matumaini yangu, Shikamoo. |

(i) __________,
S. L. P 773,
Mwanza.

05/05/2024.

Mpendwa Kaka, (ii) __________________________.

(iii) ___________________________________ kwamba wote hapo nyumbani hamjambo. Mimi sijambo na ninaendelea vizuri na masomo.


(iv) _____________________________ hii ni kukujulisha kwamba, likizo ya mwezi wa sita nitabaki shuleni ili kujiandaa na Mitihani ya Taifa. Binafsi nimedhamiria kufaulu vizuri kwa kupata gredi 'A' katika masomo yote.

Ninakutakia kila la kheri katika shughuli zako za kila siku.

(v) __________________________

Akilimali.

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 1,530,615 (100%). Swali lililenga kupima umahiri wa mwanafunzi katika kuandika barua ya kirafiki. Ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani ambapo wanafunzi 897,389 (58.63%) walipata alama 04 hadi 10. Chati Na. 4 inaonesha viwango vya ufaulu na asilimia ya wanafunzi.




**Chati Na. 4**: *Asilimia ya ufaulu wa wanafunzi katika swali la 4*

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, wanafunzi 460,772 (30.10%) walifaulu kwa kiwango kizuri sana kwani waliweza kujibu kwa usahihi vipengele vyote vitano (5) vya barua ya kirafiki ambavyo ni; anuani ya mwandishi, salamu ya awali, utangulizi wa barua, kiini cha barua na mwisho wa barua. Katika kipengele cha anuani ya mwandishi, wanafunzi waliweza kubaini kuwa (i) ni jina la shule anayosoma ambayo ni *Shule ya Msingi Ushindi*. Kipengele kingine ni salamu ya awali, katika kipengele hiki wanafunzi waliweza kubaini kuwa ndiyo sehemu inayohusisha salamu ya awali ya mwandishi wa barua kwa anayempelekea barua. Hivyo, waliweza kubaini (ii) jibu lake ni *Shikamoo.* Katika kipengele cha utangulizi wa

barua wanafunzi waliweza kubaini sehemu hiyo huhusisha maneno ya mwanzo kabla ya barua yenyewe. Hivyo, walibaini kuwa (iii) jibu lake ni *Nimatumaini yangu*.

Kipengele kingine ni kiini cha barua, katika kipengele hiki wanafunzi waliweza kubaini kuwa ni sehemu inayobeba ujumbe mkuu wa barua (madhumuni). Hivyo, waliweza kubaini jibu la (iv) kuwa ni *Madhumuni ya barua*. Vilevile, katika kipengele cha mwisho wa barua, wanafunzi waliweza kubaini kuwa huhusisha maneno ya kuhitimisha na jina la mwandishi. Hivyo, wanafunzi waliweza kubaini kuwa (v) jibu lake ni *Mimi mdogo wako*. Hata hivyo, pamoja na wanafunzi hao kufanya vizuri sana na kupata alama 10, wanafunzi 81,735 (5.34%) walifanya vizuri kwa kupata alama 08 kwani waliweza kujibu kwa usahihi vipengele vinne (4) kati ya vitano (5) walivyopewa. Kwa ujumla, wanafuzi katika kundi hili walionesha kuwa na uelewa mzuri wa dhana ya uandishi wa barua hususani katika barua ya kirafiki. Kielelezo Na. 4.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kujibu vipengele vyote vitano (5) vya swali kwa usahihi.

4. Kamilisha barua ya kirafiki ifuatayo kwa kuchagua jibu sahihi kutoka kwenye kisanduku kisha kuandika katika nafasi zilizoachwa wazi.

| |
|---|
| Mimi mdogo wako, Madhumuni ya barua, Shule ya Msingi Ushindi, Ni matumaini yangu, Shikamoo. |

(i) Shule ya msingi Ushindi.
S. L. P 773,
Mwanza.

05/05/2024.

Mpendwa Kaka, (ii) Shikamoo.

(iii) Ni matumaini yangu kwamba wote hapo nyumbani hamjambo. Mimi sijambo na ninaendelea vizuri na masomo.

(iv) Madhumuni ya barua hii ni kukujulisha kwamba, likizo ya mwezi wa sita nitabaki shuleni ili kujiandaa na Mitihani ya Taifa. Binafsi nimedhamiria kufaulu vizuri kwa kupata gredi 'A' katika masomo yote.

Ninakutakia kila la kheri katika shughuli zako za kila siku.

(v) Mimi mdogo wako
Akilimali.

**Kielelezo Na. 4.1:** Sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika swali la 4

Aidha, uchambuzi zaidi unaonesha kuwa wanafunzi 354,882 (23.19%) walipata alama za wastani kuanzia 04 hadi 06. Wanafunzi hao, waliweza kujibu vipengele viwili (2) hadi vitatu (3) kwa usahihi kwani walikuwa na maarifa yasiyojitosheleza katika kuandika barua ya kirafiki. Wanafunzi hao walishindwa kufahamu baadhi ya vipengele vya barua ya kirafiki. Wapo walioweza kuandika kwa usahihi kipengele cha anuani ya mwandishi, kiini cha barua na mwisho wa barua na kushindwa katika kipengele cha salamu ya awali na utangulizi wa barua. Katika kipengele cha anuani ya

mwandishi waliandika (i) *Shule ya msingi Ushindi*, kipengele cha kiini cha barua waliandika (iv) *Madhumuni ya barua.* Vilevile, katika kipengele cha mwisho wa barua ambapo huhusisha maneno ya kuhitimisha na jina la mwandishi waliandika (v) *Mimi mdogo wako*. Kielelezo Na. 4.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyepata alama za wastani.

4. Kamilisha barua ya kirafiki ifuatayo kwa kuchagua jibu sahihi kutoka kwenye kisanduku kisha kuandika katika nafasi zilizoachwa wazi.

| |
|---|
| Mimi mdogo wako, Madhumuni ya barua, Shule ya Msingi Ushindi, Ni matumaini yangu, Shikamoo. |

(i) Shulexamsingiushindi
S. L. P 773,
Mwanza.

05/05/2024.

Mpendwa Kaka, (ii) Shikamoo.

(iii) Madhumuniyabarua kwamba wote hapo nyumbani hamjambo. Mimi sijambo na ninaendelea vizuri na masomo.

(iv) Nimatumainiyangu hii ni kukujulisha kwamba, likizo ya mwezi wa sita nitabaki shuleni ili kujiandaa na Mitihani ya Taifa. Binafsi nimedhamiria kufaulu vizuri kwa kupata gredi 'A' katika masomo yote.

Ninakutakia kila la kheri katika shughuli zako za kila siku.


(v) Mimi mdogowako
Akilimali.

**Kielelezo Na. 4.2**: Sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyepata alama za wastani katika swali la 4

Kielelezo 4.2 kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi vipengele vitatu, kipengele cha (i), (ii) na (v) na kushindwa vipengele viwili (iii) na (iv). Hivyo, kupata alama za wastani.

Kwa upande mwingine, uchambuzi unaonesha kuwa wanafunzi 633,226 (41.37%) walipata alama za kiwango hafifu kuanzia alama 00 hadi 02. Kwani baadhi yao, wapo walioweka alama za uandishi katika nafasi iliyoachwa wazi. Wengine walinakili maneno kutoka kwenye swali husika na wengine waliweza kujibu kipengele kimoja na wengine walishindwa kujibu kwa usahihi vipengele vyote vitano (5). Kushindwa kwao kunatokana na kukosa umahiri wa kuandika barua ya kirafiki. Hivyo, kushindwa kubaini vipengele muhimu vya barua ya kirafiki. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja katika kipengele cha (i) aliandika *"Shikamoo"* badala ya "Shule ya Msingi Ushindi". Kipengele cha (ii) aliandika *"mimi mdogo wako*" badala ya "Shikamoo".

Kipengele cha (iii) aliandika "*madhumuni ya barua*" badala ya "ni matumaini yangu". Aidha, kipengele cha (iv) aliandika "*Shule ya Msingi Ushindi"* badala ya "Madhumuni ya barua" na kipengele (v) aliandika *"ni matumaini yangu".* Badala ya "mimi mdogo wako". Kwa ujumla, wanafunzi katika kundi hili hawakuwa na maarifa ya kutosha kuandika barua ya kirafiki. Kielelezo Na. 4.3 ni sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mwanafunzi katika swali la 4.



4. Kamilisha barua ya kirafiki ifuatayo kwa kuchagua jibu sahihi kutoka kwenye kisanduku kisha kuandika katika nafasi zilizoachwa wazi.

| |
|---|
| Mimi mdogo wako, Madhumuni ya barua, Shule ya Msingi Ushindi, Ni matumaini yangu, Shikamoo. |

(i) Madhumuni ya barua.
S. L. P 773,
Mwanza.

05/05/2024.

Mpendwa Kaka, (ii) Mimi mdogo wako.

(iii) Shikamoo kwamba wote hapo nyumbani hamjambo. Mimi sijambo na ninaendelea vizuri na masomo.

(iv) Nima tumaini yagu hii ni kukujulisha kwamba, likizo ya mwezi wa sita nitabaki shuleni ili kujiandaa na Mitihani ya Taifa. Binafsi nimedhamiria kufaulu vizuri kwa kupata gredi 'A' katika masomo yote.

Ninakutakia kila la kheri katika shughuli zako za kila siku.

(v) Shule ya msingi ushindi
Akilimali.

**Kielelezo Na. 4.3:** Sampuli ya majibu ya mwanafunzi yasiyo sahihi katika swali la 4

Kielelezo Na. 4.3 kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kwa usahihi vipengele vyote vitano (5) vya barua ya kirafiki. Mwanafunzi huyu hakuwa na maarifa ya kutosha ya kuandika barua ya kirafiki. Hivyo, kutoa majibu kinyume na matakwa ya swali.

## 2.5 Sehemu E: Ufahamu

Sehemu hii ilikuwa na swali moja lenye vipengele vitano (5) vyenye jumla ya alama 10. Swali lilitoka katika umahiri wa Kuonesha Uelewa wa Jambo Alilolisikiliza au Kulisoma. Swali lilipima uwezo wa mwanafunzi wa kusoma habari na kuielewa. Swali hilo ni:

**Swali la 5:** Soma kwa makini habari ifuatayo kisha jibu maswali yanayofuata kwa **kuandika jibu lililo sahihi** katika nafasi iliyoachwa wazi.

*Kalulu ni kijana anayeishi mtaa wa Kaloleni. Vijana wenzake mtaani walikuwa hawampendi kwa sababu ya tabia zake mbaya za kutowaheshimu wazazi wake, kuvuta bangi na wizi. Tabia mbaya ya Kalulu haikuishia mtaani kwake tu lakini hata shuleni aliendelea na tabia hizo. Walimu wake walijitahidi **kumrudi** lakini hakutaka kujirekebisha mwishowe alifukuzwa shule.*

*Siku moja usiku alitoroka nyumbani na kwenda kwa rafiki yake aitwaye Mashaka. Yeye pamoja na rafiki yake walikaa kichochoroni wakiwa wanavuta bangi. Polisi waliokuwa katika doria walipita katika kichochoro walichokuwa wamekaa na kuwakamata. Walipelekwa katika kituo cha polisi na hatimaye mahakamani. Hakimu alitoa hukumu na wote walifungwa katika jela ya watoto kwa miezi sita kwa kosa la kuvuta bangi na uzururaji. Baada ya kumaliza kifungo, Kalulu alibadili tabia na kuwa kijana mtiifu*

*sana. Wazazi wake na jamii kwa ujumla walimpenda na kumwamini.*

**Maswali**:

(a) Kalulu ni kijana anayeishi wapi?

______________________________________________

______________________________________________

(b) Neno **kumrudi** kama lilivyotumika katika habari uliyosoma lina maana gani?

______________________________________________

______________________________________________

(c) Kwa nini Kalulu na Mashaka walifungwa?

______________________________________________

______________________________________________

(d) Taja sababu mbili zilizofanya Kalulu kutopendwa na vijana wenzake?

(i) ______________________________________


(ii) ______________________________________

(e) Habari uliyosoma inatoa funzo gani?

______________________________________________


______________________________________________

Wanafunzi 1,530,615 (100%) walijibu swali hili. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri kwani wanafunzi 1,129,787 (73.81%) walifaulu kwa kupata alama 03 hadi 10. Chati Na. 5 inaonesha viwango vya ufaulu na asilimia ya wanafunzi.




**Chati Na. 5**: *Asilimia ya ufaulu wa wanafunzi katika swali la 5*

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa wanafunzi 231,050 (15.10%) walikuwa na kiwango kizuri sana cha ufaulu. Kwani waliweza kujibu kwa usahihi vipengele vyote vitano (5) na kupata alama 10. Wanafunzi hao walikuwa na umahiri mkubwa wa kusoma kifungu cha habari na kuelewa maudhui kwa usahihi. Hata hivyo, pamoja na wanafunzi hao kufanya vizuri sana na kupata alama 10, wanafunzi 472,739 (30.89%) walipata alama za kiwango kizuri kuanzia 6.5 hadi 9.5. Wanafunzi hao, waliweza kusoma kifungu cha habari na kujibu kwa usahihi vipengele vinne (4). Kielelezo Na. 5.1 ni sampuli ya majibu sahihi katika swali la 5.



**Maswali:**

(a) Kalulu ni kijana anayeishi wapi?

~~amy~~ anaishi mtaa wa kaloleni.

(b) Neno **kumrudi** kama lilivyotumika katika habari uliyosoma lina maana gani?

kumfundisha tabia nzuri.

(c) Kwa nini Kalulu na Mashaka walifungwa?

kwa kosa la kuvuta bangi na uzururaji.

(d) Taja sababu mbili zilizofanya Kalulu kutopendwa na vijana wenzake?

(i) kasababu ya kuvuta bangi.

(ii) kutowaheshimu wazazi wake.

(e) Habari uliyosoma inatoa funzo gani?


kuwatii wazazi wako.

kuwa na tabia nzuri.

**Kielelezo Na. 5.1:** Sampuli ya majibu mazuri katika swali la 5

Kwa upande mwingine, uchambuzi unaonesha kuwa wanafunzi 425,998 (27.83%) walipata alama za wastani kuanzia 03 hadi 06 kwa sababu walikuwa na umahiri usiokidhi matakwa ya swali moja kwa moja. Wanafunzi hao walielewa baadhi tu ya maudhui yaliyomo kwenye kifungu cha habari. Hivyo, waliweza kujibu kwa usahihi baadhi ya vipengele na kushindwa vipengele vingine. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alijibu kwa usahihi kipengele (a) *mtaa wa Kaloleni*, (c) *kwa kosa la uvutaji bangi* na *uzururaji*, (d) *kuvuta bangi* na *wizi*. Hata hivyo, alishindwa kujibu kwa usahihi kipengele (b) kwa kuandika *kwenda nyumbani* badala ya kumfanya mtu aache

tabia mbaya au kumuonya. Kipengele (e) aliandika *alikuwa mgomvi* na *alikuwa mvivu* badala ya kuvuta bangi na wizi. Hii inadhihirisha kwamba wanafunzi katika kundi hili walikuwa na umahiri usiokidhi matakwa ya swali moja kwa moja. Kielelezo Na**.** 5.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kujibu baadhi ya vipengele kwa usahihi na kushindwa kujibu kwa usahihi vipengele vingine na kupata alama za wastani.



**Maswali:**

(a) Kalulu ni kijana anayeishi wapi?

anaishi mtaa wakaloleni

(b) Neno **kumrudi** kama lilivyotumika katika habari uliyosoma lina maana gani?

Sababa kumrudi maana yake ni kurudisha kamailivyo kua.

(c) Kwa nini Kalulu na Mashaka walifungwa?

kwasababu wanavuta bangi na kuzurura mje

(d) Taja sababu mbili zilizofanya Kalulu kutopendwa na vijana wenzake?

(i) Baada ya kifungo.

(ii) Kukamata

(e) Habari uliyosoma inatoa funzo gani?


kusivute bangi

**Kielelezo Na. 5.2:** Sampuli ya jibu la wastani katika swali la 5

Kielelezo Na. 5.2 kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyepata alama za wastani kwa kuandika majibu sahihi katika kipengele (a),

(c) na (e) na kukosa kipengele (b) na (d). Katika kipengele (b) mwanafunzi aliandika maana ya “kumrudi” ni *kurudisha kama ilivyokuwa,* (d) (i) mwanafunzi aliandika *baada ya kifungo* na (d) (ii) aliandika *kukamata*.

Aidha, wanafunzi 400,828 (26.19%) walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu. Wanafunzi hao, hawakuwa na umahiri wa kuelewa maudhui ya kifungu cha habari walichokisoma. Baadhi yao walijibu kwa usahihi kipengele kimoja (1) tu kati ya vitano (5) walivyopewa. Wengine walinakili maneno yaliyopo kwenye habari waliyopewa na kujaza kama majibu ya maswali waliyopewa ambapo ni kinyume cha matakwa ya swali na kupata alama 0. Pia, katika kundi hili, wapo wanafunzi walioshindwa kabisa kujibu kwa usahihi vipengele vyote vitano (5). Kwa mfano, mwanafunzi mmoja aliandika majibu yafuatayo; Kipengele (a) aliandika *Liwale*, (b) *wazazi*, (c) *mtiifu shuleni*, (d) (i) *kuvuta* (ii) *unywaji pombe*. Aidha, kipengele (e) aliandika *kulala pazuri*. Kielelezo Na. 5.3 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu swali kwa usahihi.



**Maswali:**

(a) Kalulu ni kijana anayeishi wapi?

Nyumbani

(b) Neno **kumrudi** kama lilivyotumika katika habari uliyosoma lina maana gani?

alifukuzwa shule

(c) Kwa nini Kalulu na Mashaka walifungwa?

Mtuu wa Kaloleni

(d) Taja sababu mbili zilizofanya Kalulu kutopendwa na vijana wenzake?

(i) walipelekwa katika kituo cha polisi

(ii) Miezi sita

(e) Habari uliyosoma inatoa funzo gani?

Kalulu ni kijana anayeishi Mtuu wa Kaloleni

**Kielelezo Na. 5.3**: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 5

Kielelezo Na. 5.3 kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kwa usahihi vipengele vyote vitano. Pamoja na kwamba majibu ya mwanafunzi yametokana na habari aliyoisoma hata hivyo, majibu hayo hayaendani na matakwa ya kila kipengele katika swali husika. Hivyo, mwanafunzi huyu alipata alama 00.

## 3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WANAFUNZI KATIKA KILA UMAHIRI

Upimaji wa somo la Kiswahili umehusisha umahiri wa *kuwasiliana katika miktadha mbalimbali na kuonesha uelewa wa jambo alilosikiliza au kulisoma*. Upimaji huu ulikuwa na maswali matano ambayo yalipima uwezo wa wanafunzi wa kusikiliza na kuandika sauti mbalimbali za matamshi ya maneno katika sentensi (Imla), umahiri wa kuunda maneno mapya, kueleza maana ya nahau alizopewa, kuandika barua ya kirafiki, pia, kusoma na kujibu maswali yatokanayo na habari.

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa umahiri wa *kuwasiliana katika miktadha mbalimbali* ulipimwa katika swali la 1, 3 na 4 na ulikuwa na ufaulu wa kiwango kizuri cha asilimia 71.86. Aidha, umahiri wa *kuonesha uelewa wa jambo alilosikiliza au kulisoma* ulipimwa katika swali la 2 na 5. Umahiri huo ulikuwa na ufaulu wa kiwango cha wastani cha asilimia 63.67. Kiwango cha ufaulu cha wanafunzi kwa mwaka 2024 na 2023, kinaonesha kupanda kwa ufaulu kwa asilimia 4.02. Kutoka asilimia 64.56 kwa mwaka 2023 hadi asilimia 68.58 kwa mwaka 2024.

Aidha, viwango vya ufaulu katika mwaka 2024 vikilinganishwa na mwaka 2023 vinaonesha kuwa, katika umahiri wa *kuwasiliana katika miktadha mbalimbali,* kiwango cha ufaulu kimepanda kutoka asilimia 63.82 hadi asilimia 71.86; hivyo, ufaulu umepanda kwa asilimia 8.04. Pia, katika umahiri wa *kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza au Kulisoma*, kiwango cha ufaulu kimeshuka kwa asilimia 1.99 kutoka asilimia 65.66 hadi 63.67. Taarifa za

uchambuzi huu zimeambatanishwa kwenye **Kiambatisho Na. 1** na **2**.

## 4.0 HITIMISHO

Kwa ujumla ufaulu wa Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne katika somo la Kiswahili 2024 ni mzuri sana. Kwa sababu wanafunzi 1,293,605 sawa na asilimia 84.51 walifaulu katika upimaji huo kwa kupata alama 10 hadi 50. Wanafunzi hao walikuwa na uwezo wa kusikiliza na kuandika sauti mbalimbali za matamshi ya silabi, maneno na sentensi, kuunda maneno mapya kwa njia ya udondoshaji, kueleza maana ya nahau mbalimbali na kuandika barua ya kirafiki. Pia, walikuwa na uwezo wa kusoma na kujibu maswali yatokanayo na habari.

Aidha, jumla ya wanafunzi 236,905 sawa na asilimia 27.86 walikuwa na ufaulu hafifu. Wanafunzi hao walishindwa kujibu maswali kwa ufasaha kutokana na changamoto mbalimbali kama vile: kutokumudu stadi za kusoma na kuandika kwani walishindwa kujibu kwa ufasaha maswali yatokanayo na habari waliyopewa, athari ya lugha mama, kushindwa kuelewa matakwa ya swali, kukosa umahiri wa kuelewa nahau mbalimbali, kukosa umahiri wa kuandika barua ya kirafiki na kushindwa kuunda maneno mapya kwa kutumia njia ya udondoshaji.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Pamoja na ufaulu mzuri wa somo la Kiswahili, hatua za makusudi hazina budi kuchukuliwa ili kuboresha zaidi kiwango cha ufaulu katika Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne kwa miaka ijayo. Hatua hizo ni kama zifuatazo:

(i) Walimu wa somo la Kiswahili wawajengee uwezo wanafunzi wa kutamka na kutumia kwa usahihi sauti za herufi mwambatano kama vile; *"ng"*, "*dh*", fy'', ''*vy'' na "th"* kwenye maneno kama vile "*ng'ombe*", "dhahabu", "*fyeka*", "*vyuma*" na "thamani" mtawalia. Hii itawawezesha wanafunzi kumudu kutamka na kuandika kwa usahihi maneno yanayoundwa na sauti hizo.

(ii) Walimu wawajengee uwezo wanafunzi wa kuunda maneno mapya kwa kutumia njia ya udondoshaji wa silabi. Aidha, walimu wawajengee uwezo huo wanafunzi kwa kutumia kadi za manila na chati za maneno. Hii itawapa wanafunzi umahiri wa kuunda aina mbalimbali za maneno ya Kiswahili.

(iii) Walimu wawajengee uwezo wanafunzi wa kuwa na umahiri katika kueleza maana za nahau mbalimbali kwa kutumia njia ya maigizo, chati za maneno na vitu halisi. Hii itawapa wanafunzi fursa ya kuongeza wigo wa matumizi ya nahau katika miktadha mbalimbali.

(iv) Walimu wawajengee uwezo wanafunzi wa kufahamu vipengele muhimu katika uandishi wa barua ya kirafiki kwa kutumia chati yenye barua ya kirafiki. Hii itawawezesha wanafunzi kuandika barua ya kirafiki kwa usahihi na hivyo, kuweza kutumia maandishi katika mawasiliano kulingana na miktadha mbalimbali.

(v) Walimu wawajengee uwezo wanafunzi wa kusoma matini kwa kuwaweka katika vikundi mbalimbali ili kuwa na umahiri katika

kufahamu maudhui ya matini husika. Hii itawajengea wanafunzi uwezo wa kusoma kwa ufasaha na kuonesha uelewa wa matini aliyoisoma.

**KIAMBATISHO NA.1**

## UFAULU WA WANAFUNZI KWA KILA UMAHIRI KATIKA SFNA 2024

| Na. | Umahiri Mkuu | Ufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa Ufaulu (%) | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Namba ya swali | (%) ya Ufaulu | | |
| 1. | Kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza au kulisoma | 2 | 53.53 | 63.67 | Wastani |
| | | 5 | 73.81 | | |
| 2. | Kuwasiliana katika miktadha mbalimbali | 1 | 86.27 | 71.86 | Vizuri |
| | | 3 | 70.70 | | |
| | | 4 | 58.63 | | |

**KIAMBATISHO NA.2**

## ULINGANIFU WA UFAULU WA WANAFUNZI KWA KILA UMAHIRI KATIKA SFNA 2024 NA SFNA 2023

| Na. | Umahiri Mkuu | Upimaji 2024 | | | | Upimaji 2023 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Ufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa Ufaulu (%) | Maoni | Ufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa Ufaulu (%) | Maoni |
| | | Namba ya swali | (%) ya Ufaulu | | | Namba ya swali | (%) ya Ufaulu | | |
| 1. | Kuwasiliana katika miktadha mbalimbali | 1 | 86.27 | 71.86 | Vizuri | 1 | 85.73 | 63.82 | Wastani |
| | | 3 | 70.70 | | | 2 | 58.10 | | |
| | | 4 | 58.63 | | | 4 | 47.64 | | |
| 2. | Kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza au kulisoma | 2 | 53.53 | 63.67 | Wastani | 3 | 80.77 | 65.66 | Wastani |
| | | 5 | 73.81 | | | 5 | 50.56 | | |